

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:
Simu: 2203156/58
Fax: +25522203213
Tovuti: www.dsm.go.tz
Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA
3 Barabara ya Rashidi
Kawawa,
S.L.P 5429,
12880 -DAR ES SALAAM.
Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RC MAKONDA ATOKWA NA CHOZI, NI BAADA YA KUJIONEA MAISHA YA WASTAAFU WALIODHULUMIWA NYUMBA.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda leo ametembelea na kutoa pole kwa Familia ya Wastaafu ya Bwana Edward Bejumula na Bi. Stella Bejumula walioteseka kwa Miaka Sita bila Makazi baada ya kudhulumiwa Nyumba yao ambapo ameahidi kulivalia njuga suala hilo kuhakikisha haki inatendeka bila kuvunja sheria.

RC Makonda amewatembelea wastaafu hao na kuwapatia Msaada wa vitu mbalimbali ikiwemo Mchele, Unga, Sabuni, Ngano, Mafuta, Nyama, Viazi, Maharage, Sukari, Vitunguu, Ndizi, Nyanya kwa ajili ya matumizi ya nyumbani baada ya familia hiyo kupoteza Mali zote.

Stori ya wastaafu hao kudhulumiwa Nyumba waliyojenga baada ya kufanya kazi kwa Miaka 34 imemgusa RC Makonda hadi kujikuta anashindwa kuvumilia na kutokwa na machozi kutokana na namna inavyohuzunisha kuona mnyonge anajituma kwenye kazi na kufanikiwa kujenga nyumba halafu anatokea mtu anamdhulumu Mali yake.

RC Makonda amesema kazi ya kutafuta haki ya wastaafu hao inaanza Mara moja kwa kuwahoji watu wote waliohusika na sakata hilo wakiwemo Bank, Muuzaji wa nyumba, Mnunuzi, kampuni ya udalali ya Majembe, Watu wa Mahakama na watu wa ardhi.

Kwa sasa wastaafu hao wanaishi kwenye nyumba ya mfadhili mmoja aliyejitolea kuisitiri familia hiyo ambapo RC Makonda amemshukuru kwa moyo aliouonyesha.

Kwa upande wao Wastaafu waliodhulumiwa Mali zao wamefurahia kitendo cha RC Makonda kuona taarifa zao kwenye vyombo vya habari kisha kuwatembelea na kuwasikiliza kitendo kilichowafariji na wanaamini kwa utendajikazi wa RC Makonda wanapata haki yao.

Aidha wamemshukuru RC Makonda kwa kitendo cha kuwapelekea Chakula kwakuwa wameishi maisha ya tabu hadi kukosa vitu vya ndani ikiwemo vyakula ambapo wamemuomba kwa Mungu azidi kumpa maarifa ya kuwasaidia wananchi wanyonge.

HAKIMU WA KWELI NI MUNGU

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

27/01/2018